**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HUTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA BAJETI YA MWAKA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma aliyetujaalia kukutana asubuhi ya leo tukiwa hai na wenye afya, hii ni neema ambayo hatuna budi kuitumia vizuri katika kutekeleza aliyotuamrisha na kuitumia katika kuleta maendeleo na manufaa kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** pia napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako kwa kuliongoza vyema Baraza lako tukufu ambalo ndio sehemu tunayoitumia kwa kuwawakilisha wananchi waliotutuma kupitia majimbo mbali mbali Unguja na Pemba tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu akupeni wepesi mzidi kutuongoza vyema na kwa busara kwa manufaa ya wananchi wetu ambao matarajio yao ni kuona tunawawakilisha vyema katika chombo hichi.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile Kamati inapenda kumpongeza Waziri wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Mheshimiwa Rahma Kassim Ali na Naibu Waziri Mheshimiwa Nadir Abdul- latif Yussuf kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tunawaombea kheri na wepesi katika kutekeleza majukumu yao na kuleta tija kwa Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**Pia tunapenda kutoa shukrani kwa mashirikiano tunayopatiwa na watendaji wa Wizara hii inayoongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Joseph John Kilangi pamoja na watendaji wote ambao wamekua wakitupa ushirikiano wakati wote tunapotekeleza majukumu yetu katika kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Shukrani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati hii ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa kazi nzuri pamoja na mashirikiano makubwa wanaliyonayo katika kufanikisha majukumu waliopangiwa. Kwa mnasaba huo sasa naomba kuwatambulisha wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo :-

1. Mhe Yahya Rashid Abulla — Mwenyekiti
2. Mhe Hudgaima Mbarak Tahir — Makamo Mwenyekiti
3. Mhe Mussa Foum Mussa — Mjumbe
4. Mhe Bahati Khamis Kombo — Mjumbe
5. Mhe Kombo Mwinyi Shehe — Mjumbe
6. Mhe Hussein Ibrahim Makungu — Mjumbe

Aidha, kamati hii ina makatibu wawili ambao wamekua wakitupata msaada na kuhakikisha tunafanikisha majukumu yetu kama inavyotakiwa. Naomba nao niwatambue kama ifuatavyo;-

1. Ndg. Rahma Kombo Mgeni — Katibu
2. Ndg. Himid Haji Choko — Katibu

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo kwa mujibu wa kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2020 kanuni ya 107(3) tumeweza kufanikisha kufatilia na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali ikiwemo hii ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi yenye Fungu **N02** inatekeleza majukumu yake kupitia programu kuu Tatu (3) na Programu ndogo Tano (5)ambazo zinasimamiwa kupitia Idara mbali mbali zilizochini ya Wizara hii kwa lengo la kuleta maendeleo na kutatua changamoto zote ziliopo katika masuala mazima ya Ardhi na Makaazi.

**Mheshimiwa Spika**, ***Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi*** ina jukumu la kuimarisha uratibu katika utekelezaji wa kazi za Wizara kwa Unguja na Pemba. Kamati inapongeza Wizara kwa kukamilisha Rasimu ya mpango mkakati wa miaka mitano (5) wa Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Mipango kwa ajili ya kupata maoni na kuwasilishwa kwa wadau na kupata maoni kabla ya kuanza kutumika.

Vile vile,Kamati kupitia program hii inaishauri Wizara kufanya jitihada za makusudi kwa mwaka wa fedha ujao kwa kurekebisha Sera na Sheria zote ziliopo chini ya Wizara yao ambazo zinakwaza utekelezaji wa majukumu yao kwa lengo la kuleta na kuimarisha utoaji wa huduma zao na kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. lakini pia Kamati inaishauri Wizara kujikita katika kufanya tafiti zenye tija kwa nchi katika maeneo ya mipango miji na vijiji pamoja na masuala mazima ya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,**Vile Vile kupitia Idara ya Mipango Sera na Utafiti Kamati inasisitiza kukamilishwa Sera mpya ya Mipango Miji na Vijiji ambayo itasaidia kuweka mipango mizuri ya Mji wetu na kupelekea kuwa na Miji iliyopangwa vizuri na kuleta haiba nzuri ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati imefarajika na hatua inayoendelea ya utekelezaji wa Mradi wa **MKURABITA** ambao upo chini ya Kamisheni ya Ardhi wenye lengo la kutambua na kusajili ardhi yote ya Zanzibar kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi. Kamati inaamini kwamba iwapo hatua hii itaweza kufanikishwa kama ilivyokusudiwa basi itaweza kusaidia sana kutatua changamoto ziliopo katika masuala mazima ya ardhi ambapo zimekua zikiongezeka siku hadi siku na kuleta athari za migogoro ya Ardhi kama inavyoonekana katika jamii na nchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa Upande wa Wizara ya Ardhi Pemba bado Kamati inaendelea kusisitiza na kuagiza kuchukuliwa hatua za makusudi kwa mwaka wa fedha ujao ili kutatua changamoto zinazoikabili Wizara zikiwemo ufinyu wa bajeti, upungufu wa wafanyakazi, wataalamu kama vile wapimaji ardhi,wapangaji miji,maafisa wa ardhi, wathamini wasaidizi, wapimaji na mainjinia. Vile vile, upungufu wa vitendea kazi ikiwemo magari na vifaa vya upimaji hali ambayo inapelekea upungufu katika ukusanyaji wa mapato. Changamoto hizo tulizozibainisha zinapelekea kuzorotesha utekelezaji wa malengo ya Wizara waliojipangia.

**Mheshimiwa Spika,***Katika Program Kuu ya Usimamizi wa Ardhi,*Kamati kupitia programu hii inashauri Wizara kuchukua jitihada za makusudi na kusimamia masuala yote ya ardhi kupitia Mahkama ya Ardhi na Kamisheni ya Ardhi ili kuweza kuondosha changamoto zinazoikabili Wizara. Masuala ya migogoro ya ardhi yamekua ni kilio cha muda mrefu ambapo kimesababisha hasara na athari kubwa kwa jamii na nchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mahakama ya Ardhi, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya Bajeti ndogo ambayo haikidhi haja kwa shughuli za Mahkama ya Ardhi pamoja na kiwango kidogo cha upatikanaji wa fedha ambacho husababisha kutofikiwa malengo waliojipangia.Kamati inashauri kwa mwaka wa fedha ujao kutengwa fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa Mahkama na kuingizwa kwa wakati ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia Kamisheni ya Ardhi, kamati inapongeza azma iliopo ya utambuzi wa ardhi yote ya Zanzibar amabyo itakua ni suluhisho katika kuondosha changamoto za migogoro ya ardhi,umiliki wa ardhi lakini pia itasaidia katika upangaji mzuri wa miji yetu, Kamati inaomba Serikali kuwezesha kufanikisha zoezi hili la utambuzi wa ardhi kwa kuwapatia fedha ambazo zitawezesha kufanikisha kazi hiyo itakayosaidia kuondosha changamoto nyingi katika masuala ya ardhi kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na nia njema na nzuri ya Serikali katika suala zima la udhibiti wa mapato ya serikali kupitia malipo yanayofanywa kwa Kamisheni katika upimaji wa ardhi kuingia katika mfuko Mkuu wa Hazina, Kamati inahisi utaratibu huu umekua unakwaza kidogo katika ufanisi wa utekelezaji wa kazi za kamisheni kwani wanashindwa kufanikisha kazi zao kutokana na kukosekana kwa fedha za kufanyia kazi hizo.

Hivyo, kamati inaishauri Wizara ya Ardhi kufatilia suala hili kwa Wizara ya fedha ili ziweze kupatikana fedha hizo ambazo zitatumika katika kukamilisha kazi za Kamisheni na kuondosha usumbufu uliopo sasa wa kazi nyingi za upimaji kuchukua muda mrefu kutokana na ukosefu wa fedha na kupelekea malalamiko kwa waliofanya malipo ya kazi zao.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati inashauri Wizara kuliangalia suala zima la changamoto kubwa ya usafiri kwa bajeti hii kwa Afisi zake za Unguja na Pemba ambalo pia linapelekea kukwaza kazi za upimaji ardhi lakini pia kununuliwa kwa vifaa vya upimaji ili zoezi la upimaji liweze kufanikiwa kama lilivyokusudiwa kwani itakua aibu iwapo zoezi hili litasuasua kutokana na ukosefu wa vifaa kwa mwaka wa fedha ujao na kushindikana kukamilika malengo mazuri yaliyokusudiwa na Serikali katika Wizara hii.

**Mhshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kwa kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo hadi kufikia Machi imeweza kukusanya milioni 132.392 sawa na asilimia 265 kwa jitihada hizo Kamati inaitaka Afisi hii kuongeza jitihada Zaidi ya kuhakikisha inaaendeleaa kukusanya mapato Zaidi kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,**hata hivyo, Kamati inaisisitiza Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kukamilisha mfumo wa kieletroniki kwa mwaka ujao wa fedha kwa lengo la kuingiza taarifa za mali zilizofanyiwa uthamini ili kuwe na kumbukumbu rasmi ambayo itasaidia kuhifadhi taarifa zote za kazi zinazofanywa na Afisi hiyo. Aidha, kukamilika kwa mfumo huo utasaidia kuwepo kwa taarifa ambazo kwa sasa zinakosekana.

**Mheshimiwa Spika,*****Programu Kuu ya Maendeleo ya Makaazi,***programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa makaazi salama na endelevu kwa wananchi na watumishi wa ngazi zote za Serikali pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa sekta binafsi katika huduma ya makaazi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Wakala wa Majengo, kamati inatoa wito kwa Serikali kuwatumia Wakala wa Majengo katika hatua za awali za uandaaji wa Miradi yao ili waweze kutoa ushauri kitaalamu na kuweza kusaidia kufanikisha Miradi ya Serikali na kuwa na ubora unaotakiwa. Hatua hii ya ushirikishwaji huenda ikawa ni suluhisho ya changamoto kadhaa zinazojitokeza wakati wa utekelezaji hasa ongezeko la gharama kutokana na mapungufu yanayojitokeza katika usanifu wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile,Kamati inaisisitiza Wizara kuchukua jitihada za makusudi kwa bajeti ijayo kulichukulia hatua suala la kuwapatia ofisi Wakala wa Majengo kwani wamekua wakisumbuka kwa muda mrefu sasa kwa kukosa ofisi za kudumu.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati inasikitishwa na maendeleo ya Shirika la Nyumba kwani limekua likijikongoja na kujiendesha kwa hasara sana na kupelekea kusuasua katika kufikia malengo ya kuundwa kwake ambapo hali hii tumeibaini inasababishwa na mambo mbali mbali yakiwemo kutokua na fedha za kujiendesha ambazo kwa asilimia kubwa zinategemewa kutokana na malipo ya kila mwezi katika nyumba wanazomiliki Unguja na Pemba. Aidha, Kamati imegundua hali mbaya sana ya malipo hayo kwa waliokodishwa ambapo inapelekea kuzorota kwa malengo yote waliojipangia.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati inasisitiza na kuwataka wale wote waliokodishwa kulipa kwa wakati ili Shirika liweze kufanya kazi zake ikiwemo ukarabati wa nyumba zake lakini pia kuondoshwa muhali na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu kwa wale wote wasiotaka kulipa madeni yao.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inalitaka Shirika kuwa wabunifu kwa Miradi mipya na yenye kuleta tija kwa Serikali ambayo itasaidia kupatikana kwa fedha za kuliendesha Shirika na kuleta tija kwa Nchi yetu. Vile vile mbali na makusanyo yatokanayo na kodi za nyumba, Kamati inaishauri Serikali kuliongezea nguvu Shirika ili liweze kujiendesha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla kamati imesikitishwa na hali isiyoridhisha ya upatikanaji wa fedha za matumizi na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ilipangiwa kutumia **Tzs Bilioni 19.117** kati ya fedha hizo **Tzs Bilioni 8.807** kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi ,2022 Wizara ya Ardhi na Mendeleo ya Makaazi imeripoti kupatiwa **Tzs Bilioni 4.392** kwa kazi za kawaida na mishahara ambazo ni sawa na **asilimia 50** na kwa upande wa kazi za maendeleo kamati imejuilishwa kuwa hakuna fedha iliyopatikana. Hivyo kufanya fedha zote zilizopatikana kuwa ni **Tzs Bilioni 4.392** sawa na asilimia **23** tu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na upatikanaji huo mdogo wa fedha imepelekea kutokamilika kwa malengo mingi ya Wizara waliojipangia kupitia Idara na Taasisi ziliopo chini yake na kushindwa kufanikisha kama walivyokusudia.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii kwa kweli inarudisha nyuma jitihada za watendaji wetu na pia kuzotesha upatikanaji wa huduma kwa jamii na maendeleo kwa nchi yetu. Hivyo, Kamati inataka Serikali kuhakikisha kwa mwaka wa fedha ujao 2022/2023 upatikanaji wa fedha uwe kama unavyopangwa na kuingizwa kwa wakati ili basi Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi iweze kukamilisha malengo yake kwa ufanisi na kuleta maendeleo yaliyokusudiwa kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika;**
Aidha, mipango yote iliyomo katika Bajeti hii ya 2022/2023 haitoweza kutekelezeka ikiwa makusanyo ya mapato hayatafanyika kama ilivyokusudiwa kwa Taasisi zote ambazo zinahusika moja kwa moja na ukusanyaji wa mapato. Kamati inawaomba wale wote waliopewa majukumu ya ukusanyaji wa mapato katika Wizara hii kufanya kazi kwa bidii na uadilifu ili kufikia malengo ya ukusanyaji kama walivyokadiria.

**Mheshimiwa Spika;**
Mwisho kabisa, ili kufikiwa malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, kwa niaba ya Kamati yangu tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie na wairidhie Bajeti hii na hatimae waidhinishiwe jumla ya fedha zote zilizopangwa kutumika kwa mwaka wa fedha *2022/2023* kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;**

*Kwa niaba ya Kamati yangu **Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,

……………..………………..
(Yahya Rashid Abdulla)
Mwenyekiti,

KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR